

Ninaelewa, kwa hiyo, Ninaamua na Kuchagua: Demokrasia, Kiswahili na Maendeleo ya Wananchi wa Tanzania

Aldin Mutembei
Profesa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

kaimutembei@gmail.com

Ikisiri

Makala inachambua dhana ya demokrasia, lugha ya Kiswahili, na maendeleo ya wananchi. Inaangalia demokrasia inavyoweza kujengwa na lugha; na kuwafanya wananchi kujitambua na kuchukua hatua kujiletea maendeleo. Makala inajadili kuwa, mosi, jitihada za kuwafanya wananchi waweze kushiriki katika mchakato wa kidemokrasia lazima zilenge kuwafanya wananchi hao kuelewa kile wanachokitaka wao wenyewe. Pili, ili kufanikisha ukombozi wowote, ni lazima wananchi wawe na uelewa wa kifikra na kujitambua. Kuelewa na kujitambua hufanikishwa kupitia mawasiliano yanayotokana na lugha inayochipuka katika mazingira na utamaduni wa wananchi husika. Bila kuelewa hakuna kujitambua, na itakuwa vigumu kushiriki katika demokrasia. Bila kuelewa hakuna maendeleo. Bila mtu kuweza kuyaelewa mazingira yake na kuyamudu, hakuwezi kukawa na ukombozi wa kweli. Kieneo, makala hii imekitwa nchini Tanzania kama kiwakilishi cha maeneo mengine yanayotumia lugha ya Kiswahili barani Afrika. Makala inatumia Nadharia ya Ubaadukoloni katika kujadili dhana ya demokrasia kwa kutumia mkabala wa lugha ya Kiafrika. Tutaonesha kuwa lugha ya Kiswahili inaweza kuwapatia wananchi uelewa na kuwasaidia kushiriki kikamilifu katika kujenga na kuimarisha demokrasia. Tunalenga kuonesha kuwa, kupitia lugha inayoeleweka, wananchi wataimarika kidemokrasia na watashiriki katika kujiletea maendeleo.

Dhana za Msingi: Demokrasia, maendeleo, Kiswahili, ukombozi

Utangulizi

Moja ya malengo ya elimu ya kujitegemea (Nyerere, 1967) ilikuwa kumfanya mtu kuyamudu mazingira yake. Falsafa ya elimu ya kujitegemea ilikusudia kumfanya mtu atafakari kuhusu ukombozi unaoanzia katika fikra yake (Nyerere, 1967). Nchini Tanzania, misingi ya elimu ya kikoloni ililenga kuwapa wananchi wachache elimu itakayowawezesha kuendelea kuwatumikia na kuwategemea wakoloni (Nyerere, 1974). Ni kwa kiasi gani baada ya miaka hamsini ya kuwa huru Tanzania imejinasua kutoka misingi hiyo, ni suala la mjadala. Wakati wa ukoloni, haikuwapo elimu ambayo ililenga kuwafanya wananchi wajitambue na kujiletea mabadiliko. Ilikuwa ni elimu iliyopumbaza. Isiyomwandaa mtu kujisaka, kujijua, kujiheshimu na kujithamini. Kuitukuza lugha ngeni na kuibeza ile ya wenyeji ilikuwa ni moja ya silaha zilizotumika katika kumpumbaza Mwafrika. Mazrui na Mazrui (1998) wanadai kuwa suala la lugha halikufanana kwa wakoloni wote, hivyo, haipaswi kuelezwa kama kwamba wote walikuwa na sera ileile. Hata hivyo, jambo ambalo kwa wakoloni wote lilikuwa sawa, ni dharau kwa watawaliwa na kubeza lugha zao. Ni kweli kuwa tafiti za wakoloni kuhusu lugha za Kiafrika zilizifanya lugha hizo kutambulikana na kuwapo kwa maandishi yaliyojenga tafiti nyingine za baadaye kuhusu lugha hizo. Nia ya tafiti hizo pamoja na sababu nyingine ilikuwa hatimaye kuwarahisishia wakoloni utawala na unyonyaji. Sababu nyingine zilikuwa kuchunguza na kujua Ontolojia, mitazamo, na imani za wenyeji; na kuweza kufanya mawasiliano na wenyeji (Mulokozi, 2019:20-21). Pamoja na hali hiyo, hakuna ushahidi wa kutosha kuonesha kuwa wakoloni walijenga misingi ya kidemokrasia katika makoloni yao kwa kuihusisha misingi hiyo na lugha za wenyeji.

Utafiti kuhusu uhusiano kati ya lugha za wenyeji na demokrasia umefanywa na wataalamu mbalimbali. Brock-Utne (2002) anaangalia lugha katika muktadha wa utandawazi na kujadili uhusiano wake na masuala ya haki za kijamii na kidemokrasia. Hoja yake ni kuwa mifumo ya utolewaji maarifa katika Afrika, kwanza, imejengwa katika utamaduni na mila za Kiulaya, na pili, maarifa yanatolewa kupitia lugha za Ulaya. Anasisitiza kuwa ikiwa viongozi wanajali haki za kijamii na kidemokrasia, basi hawana budi kuzijenga na kuziimarisha lugha za Kiafrika (Brock-Utne, 2002: 6). Yakubu (2016) anajadili kuwa, ingawa nchi za Kiafrika zinadai kuwa na demokrasia, baadhi zimeshindwa kuwapatia wananchi wake maendeleo. Akifafanua uhusiano baina ya maendeleo na demokrasia, anasema kuwa, demokrasia humfanya mtu kuchagua kiongozi amtakaye, husababisha uchumi wa kiliberali, na kurahisisha uhuru wa kushirikiana. Fosu (2020) anaonesha kuwa, katika Afrika, kumekuwa na tafiti mbalimbali zilizolenga kuonesha uhusiano baina ya maendeleo na demokrasia. Anasema kuwa kutokuwapo kwa uongozi bora kumekuwa ni kikwazo katika maendeleo ya nchi za Kiafrika. Anaonesha kuwa uchaguzi wa viongozi bora unaweza kusababisha maendeleo kutokana na sera mwafaka za uongozi na kuinua uchumi. Hata hivyo, Yakubu (2016) na Fosu (2020) hawaoneshi kuwa haya yote hayawezi kufanyika kwa ufanisi pasipokuwa na lugha inayotoa nafasi ya mawasiliano na kuelewana. Suala la lugha inayoeleweka kwa wote linachukuliwa kijuujuu, kama jambo linalojieleza bila kuwapo na ulazima wa kulijadili.

Katika kazi yake nyingine, Brock-Utne (2004) anaangalia sera za lugha katika Afrika. Anajadili lugha ya kufundishia katika elimu ya juu na kuihusisha na demokrasia. Katika makala yake, anaonesha kuwa uamuzi wa

lugha ipi iwe ya kufundishia ni wa kitabaka. Tabaka la juu, lenye watu wachache linapendelea lugha za kikoloni kutumika katika elimu ili liendeleo kufaidi mifumo ya maarifa na kuhodhi demokrasia kwani wanaofahamu lugha hiyo ni wachache tu. Wakati huohuo, tabaka la chini lenye watu wengi linaendelea kutokuwa na maarifa wala sauti katika masuala ya utawala, kwani maisha duni hayaliwezeshi tabaka hili kumudu gharama za juu za elimu inayotolewa katika lugha za kikoloni. Ni muhimu kufahamu lugha inavyohusiana na demokrasia ili kuweza kujadili umuhimu wa matumizi ya lugha za Kiafrika katika kujenga demokrasia itakayokuwa na maana na kuleta ufanisi katika Afrika. Hii inamaanisha kuwa, si lazima kuwe na demokrasia ya aina moja duniani kote. Mwalimu Julius Nyerere akifafanua hoja kama hii, aliwahi kusema kuwa “demokrasia si chupa ya Coca-Cola ambayo unaweza kuiagiza kutoka nje” (Nyerere, 1991). Hapa alimaanisha kuwa demokrasia haina budi iendelezwe na wananchi ikiendana na maisha na matakwa yao wenyewe. Kwa mawazo haya, demokrasia haiwezi kufanana katika jamii zote duniani. Mawazo haya yanaendelezwa na Osabu-Kle (2008) anapoichambua demokrasia ya kiliberali na kusema kuwa serikali za Kimagharibi zinahubiri mfumo wao wa demokrasia kama dini kwa dunia nzima na hasa kwa Afrika kupitia mashirika ya KiBreton Woods. Hata hivyo, Osabu-Kle (2008) anasema kuwa kuna mambo yanafanana kati ya demokrasia hii ya kiliberali na udikiteta (Osabu-Kle, 2008:4). Anasema kuwa, demokrasia hii ya Kimagharibi ni ya kinafiki, na sio tu haifai bali pia haiwezi kuwakusanya watu wengi pamoja ili watambue yale wayatakayo, watimize ndoto zao na kufanikisha matamano yao. Anaona kuwa demokrasia ya kiliberali inafaa katika mfumo wa Kibepari (Osabu-Kle, 2008:5). Kwa mawazo yake, demokrasia inayofaa kwa nchi za Kiafrika ni ile ya utamaduni unaoendana

au kupatana. Demokrasia hii anayoita demokrasia ya kukubaliana au Jaku¹ ilikuwapo Afrika kabla ya kuvamiwa na wakoloni (Osabu-Kle, 2008:11) kama tutakavyoona katika sehemu inayofuata. Hata hivyo, katika mjadala wa Osabu-Kle, kama mijadala ile mingine tuliyoionesha (Fosu, 2020; Yakubu, 2016; na Mazrui na Mazrui, 1998), bado kiungo kinachokosekana ni lugha inayoweza wananchi kusikilizana na kufanya maamuzi.

Ili kufuatana vizuri katika kufahamu umuhimu na nafasi ya lugha katika kuijenga na kuiimarisha demokrasia, tunapendekeza katika makala hii, tuanze na ufafanuzi wa dhana ya demokrasia kietimolojia. Lengo la kufanya hivi ni kuonesha wazi jinsi gani demokrasia inavyojengwa na lugha, kama moja ya mihimili yake mikuu. Katika kufafanua huku, makala hii inatumia Nadharia ya Ubaadaukoloni ikionesha uhusiano wa dhana ya demokrasia na lugha na jinsi maendeleo ya kweli ya Afrika yanavyotakiwa kuwa na mkabala tofauti wa demokrasia. Sehemu ifuatayo inaeleza kwa kifupi Nadharia hiyo ya Ubaadaukoloni.

Kiunzi cha Nadharia

Utafiti umeongozwa na Nadharia ya Ubaadaukoloni. Ubaadaukoloni ni mawazo na mjadala hasa wa kisomi unaoonesha mwitiko wa jamii na uchambuzi wake kuhusu athari za ukoloni, ubeberu na mabaki yake katika utamaduni wa watu waliotawaliwa. Inaangalia pia kujinasua na ubaada ukoloni huo. Mawazo haya hugusa uhusiano na kufanana kwa mambo baina ya watawaliwa na wale waliowatawala, na katika jamii zilizotawaliwa (Homi, 1994; Comaroff na Comaroff, 1997; Chandra, 2013; Ballestrin, 2014; Elam, 2019). Katika mawazo haya, Elam anaongeza kuwa, ni vigumu

¹ Jaku Democracy inaelezwa kuwa ni demokrasia iliyochipuka Afrika kabla ya wakoloni ambapo majimbo (mataifa kabla ya mgawanyo wa sasa wa kikoloni) yalikuhaliana kuhusiana na uamuzi fulani kwa mustakabali wa jamii.

kuzungumzia, “Falsafa ya Ulaya”, au “Fasihi ya Ulaya” au hata “Historia ya Ulaya”, kama dhana zinazojitegemea bila kuhusisha kuwapo kwa ukoloni na unyanyasaji wake katika dunia.

Katika nadharia hii, makala yetu inaangalia dhana ya demokrasia inavyoangaliwa baada ya ukoloni. Mawazo ya Ballestrin ni kuwa Nadharia ya Ubaadaukoloni imeshindwa kuifafanua demokrasia kwa mtazamo wa kibaada ukoloni kwa jinsi ileile nadharia mbalimbali kuhusu demokrasia zilivyoshindwa kuunga mkono mitazamo ya demokrasia baada ya ukoloni (Ballestrin, 2014: 213 - 218).

Kati ya wanazuoni wengi waliojadili kuhusu Ubaadaukoloni (Samir, 1977; Said, 1978; Homi, 1983, na 1994; Ashcroft, Griffiths, na Tiffin 1995; Comaroff na Comaroff, 1997; Chandra, 2013; Ballestrin, 2014; Elam, 2019) ni wachache sana walihusisha suala la lugha na ukoloni. Kwa mfano, Fanon (1986) anasema wazi kuwa wakoloni walitumia lugha zao kutawala na kuwafanya watawaliwa kupoteza lugha zao za asili. Wanadai kuwa kuzungumza lugha za kikoloni ni kushiriki katika dunia na kuasidi ustaarabu (Fanon, 1986:1-18). Kwa wakoloni, ni lugha zao pekee ndizo walizoziona kuwa zina maana ya kuumba ulimwengu. Lugha hizo walizieneza kwa namna mbalimbali katika makoloni yao, aghalabu, kwa kutumia nguvu. Suala la lugha wameliongelea pia Ngugi (1981) na Kezilahabi (2012) katika muktadha wa Fasihi za Kiafrika. Ngugi (1981) anaeleza kuwa ni muhimu kwa wanafasihi wa Kiafrika kujivua fikra za kikoloni pale wanapoandika kazi za kifasihi. Kwa upande wake Kezilahabi (2012), anaonesha kuwa wakoloni walilenga kufifisha Uafrika kwa kutokutambua fasihi zilizoandikwa katika lugha za Kiafrika.

Katika hoja tunazoziona hapa juu kuhusu Ubaadaukoloni, mjadala unaonesha jinsi lugha za kikoloni, hasa katika Afrika zilivyoathiri fikra ya Mwafrika na zinavyoendelea kumdunisha. Hatua za maendeleo haziwezi kuonekana katika uduni huo. Na mawazo ya kidemokrasia hayawezi kuibuka katika fikra duni zinazobeza uasili na utambulisho wa mtu. Ili kujadili kwa kina uhusiano wa dhana ya demokrasia na lugha na kisha kuonesha jinsi vipengele hivi viwili vinavyohusiana na maendeleo, hatuna budi kujadili dhana ya demokrasia kietimolojia.

Tunachambua dhana ya demokrasia kietimolojia kutoka katika lugha ya Kiyunani ambako ndipo istilahi hii inapochipukia. Baada ya hapo, tunaendeleza mjadala wetu tukiirejelea lugha ya Kiswahili na jinsi inavyohusika na ujenzi wa demokrasia katika Tanzania. Tunaonesha changamoto katika kukua kwa demokrasia kwa kutumia mkabala wa lugha. Tunajadili demokrasia kwa muktadha wa Tanzania, huku tukiangalia uhusiano wake na dhana ya maendeleo ya Watanzania. Tunaunganisha maarifa kutoka katika maana ya demokrasia na maarifa katika hadhi ya Kiswahili huku tukijadili umuhimu wa dhana hizi katika kuleta maendeleo ya Tanzania. Suala la demokrasia, ni suala la uelewa na kuchukua uamuzi wenye urazini. Hivyo, ni suala linalogusa fikra ya mtu. Tatizo la mtu kutokuelewa kinachozungumzwa, inasababisha pia asielewe kinachotendeka. Lugha za kikoloni kama Kifaransa, Kiingereza na Kireno zililazimishwa katika makoloni ilihali wananchi hawakuwa na uelewa wa kina wa lugha hizo ambazo hazina mizizi katika jamii zao. Kwa hiyo, wananchi walilazimika kufanya uamuzi bila uelewa unaochipuka katika lugha za asili. Wananchi walio wengi ambao hawakuwa na uelewa wa kina, sio tu walifikwa na tatizo katika fikra, lakini zaidi kwa kuwa wao wenyewe

walikuwa wanabeza lugha zao za asili, walihitaji kukombolewa. Kutokueleweka kwa lugha kuliwafanya wawe kama watumwa wanaofuata tu matakwa ya bwana wao bila uelewa na utashi. Tunamaliza mjadala wetu kwa maswali ya ni nini kinahitajika kwa Watanzania ili kuwa na ukombozi utakaotuondolea ufukara na unyonge wa kifikra. Tukipata uelewa huu, ni matazamio yetu kuwa tutaweza sio tu kushiriki katika kuchagua viongozi bora, bali zaidi tutaweza kutetea kwa nguvu zote, harakati zozote za kufakamiwa na kuporwa kwa rasilimali zetu. Tutaweza kushiriki vizuri katika ujenzi wa elimu bora Tanzania. Elimu itakayotuletea maendeleo ya kweli.

Methodolojia

Makala hii imetokana na utafiti wa kimaktaba. Imeegemea katika mbinu ya uchambuzi wa kitaamuli kama ilivyofafanuliwa na Onwuegbuzie, Leech, na Collins (2012). Katika maelezo yao, uchambuzi wa kitaamuli humfanya mtafiti kutafuta dhana kutoka katika machapisho na nyaraka mbalimbali zinazoeleza na kufafanua jambo analolitafiti.

Katika makala hii, tulitumia maktaba ya Wilbert Chagula ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na hasa kusoma machapisho yanayofafanua etimolojia ya neno “demokrasia”. Aidha machapisho mengi yalipatikana mkondoni. Kwa kutumia injini tafutizi kama vile *Google*, tuliweka dhana ya msingi tunayoitafula na kupata machapisho yanayohusiana na dhana hiyo. Onwuegbuzie na wenzake (2012) wanaeleza kuwa usomaji wa machapisho ni hatua moja, lakini kusoma kwa kina chapisho linaloelekeana zaidi na dhana inayotafutwa ni suala la msingi. Kupitia katika usomaji wa kina, dhana za msingi katika makala yetu, zilichambuliwa. Uchambuzi huo pia uliangalia kuhusiana kwa dhana hizo ili kuweka ushikamani wakati wa

kujenga mjadala. Katika uchambuzi huu, tumelazimika kuangalia dhana ya demokrasia katika Afrika ya kale kabla wakoloni hawajavamia na kuitawala Afrika kwa kuingiza mawazo na fikra zao kuhusu dhana hizo. Aidha, kupitia katika uchambuzi huo, baada ya kuangalia kwa kifupi dhana ya demokrasia ilivyokuwa katika Afrika, tuliangalia dhana hii kutoka Uyunani ambako neno “demokrasia” linaibuka. Uchambuzi wa Afrika ya kale na Uyunani umeegemea katika lugha na fasihi simulizi, hasa tukizichambua semi zinazohusiana na dhana ya demokrasia. Baada ya uchambuzi wa lugha na semi, mjadala wetu umeangalia uhusiano wa lugha ya Kiswahili na dhana ya demokrasia na kuonesha jinsi kufahamu lugha kunavyohusiana na uchaguzi. Hatua hizo za uchambuzi ndizo tulizoziita: “Ninaelewa, Kwa hiyo, Ninaamua na Kuchagua” tukimaanisha kuwa uamuzi na uchaguzi hutokana na kuwapo kwa mawasiliano baina ya watumiaji wa lugha lengwa. Sehemu zifuatazo zinalenga kuonesha hatua hizi na kudokeza mjadala unaonesha uhusiano baina ya demokrasia, lugha na maendeleo.

Matokeo ya Utafiti

Mjadala wa makala hii utajikita katika Demokrasia katika Afrika ya Kale; Demokrasia ya Uyunani ya Kale; Kiswahili na Ujenzi wa Demokrasia; na Lugha na Maendeleo.

Demokrasia katika Afrika ya kale

Wakati tukianza mjadala wa etimolojia ya demokrasia kama ilivyojulikana kwa Wayunani, hatuna budi pia, angalau kwa kifupi tu, tuangalie ikiwa dhana hii ya demokrasia ilikuwapo Afrika kabla ya majilio ya wakoloni, na jinsi dhana hiyo ilivyojitokeza katika tamaduni na maisha ya watu wa Afrika. Kutokana na maandishi machache yaliyopo, inajulikana kuwa utaratibu ambao leo unaitwa demokrasia, ulikuwapo Afrika kabla ya

kuvamiwa na wakoloni. Kule Nubia na Misri ya Kale, Diop (1974), anatuonesha jinsi mila ya uchaguzi na uwakilishi iliegemea katika uelewa wa wananchi, ambapo kwa kutumia lugha ambayo wote waliielewa walichagua wawakilishi wachache kuwasemea waliokuwa wengi.

Osabu-Kle (2008) anafafanua zaidi kuwa dhana ya demokrasia si ngeni kwa Afrika. Ilikuwapo Afrika ikiwa ni sehemu ya utamaduni wa makubaliano na ilijitokeza katika mifumo ya upangaji kazi na katika shughuli za kiushirika. Anasema kuwa wananchi walizoea kukutana chini ya vivuli vya miti na katika sehemu za wazi, iwe ni uwanjani au mashambani. Katika kukutana huko, wananchi walikubaliana kuchagua wawakilishi watakaowasemea kuhusu mambo ya uchumi au siasa kutegemea walivyokubaliana. Hii ingeweza kuitwa “Demokrasia” ya makubaliano (Osabu-Kle, 2008:10). Kupitia demokrasia ya makubaliano, wanajamii walikuwa na mchakato wa uchaguzi. Koo ziliungana kujadili mambo ya vijiji, na vijiji viliungana kuzungumzia mambo ya miji. Katika mifumo hiyohiyo, vijiji na miji iliungana kuwa na dhana ya taifa. Mtaalamu huyu ameendelea kufafanua kuwa muundo huo wa demokrasia ya mila au utamaduni wa kupatana au kukubaliana ulijitokeza katika Himaya za kale za Afrika zilizokuwa Misri ya Kale, Ghana, Mali, na Songhai kabla Afrika haijavamiwa na wakoloni. Mbali na Kaskazini Magharibi na Kati mwa Afrika, Osabu-Kle (2008) anaonesha kuwa utaratibu kama huo ulikuwa pia katika Himaya za Monomotapa katika Falme za Zimbabwe na Himaya za Kizulu kule Kusini mwa Afrika.

Akijiegemeza katika mkabala wa lugha na fasihi, Kabongo (1986) anaonesha jinsi demokrasia ilivyokuwa miongoni mwa jamii ya Waluba wa Kongo kabla nchi hiyo haijakaliwa na wakoloni. Msemo katika lugha ya

Kiluba kuwa; *Mukalenge wa Bantu, Bantu wa Mukalenge*, (yaani Mfalme huwapo kwa ajili ya watu, na watu kwa ajili ya Mfalme) unadhihirisha utamaduni wa kidemokrasia miongoni mwa Waafrika wa Kongo. Aidha, Magang (1986) anatuonesha dhana ya demokrasia miongoni mwa Watswana kabla ya uvamizi wa wakoloni. Utaratibu wao uitwao *lekgotla* uliendana na msemo kuwa: *Mfalme ni mfalme kutokana na utashi wa watu*. Yapo maandishi mengi kama ya Busia (1967), Kaba (1986), na Mangu (2006), kwa kifupi, yanayotunesha na kudhihirisha kuwa dhana ambayo sasa inaitwa “demokrasia” chanzo chake kwa hakika ni hapa Afrika. Kwa hiyo, Waafrika hawapaswi kufuata mikabala na viunzi vya kidemokrasia vya Kimagharibi yaani Ulaya, au Marekani au hata Asia. Kutokana na kutawaliwa na mataifa ya Ulaya, na kutokana na kutokuwapo kwa kumbukumbu nzuri, demokrasia inadhaniwa kuwa ni dhana iliyochimbuka kutoka Ulaya – Ugiriki au Uyunani ya kale. Maandishi mengi yanaonesha hivyo huku suala la uasili wa Afrika likiachwa bila kujulikana.

Kwa kuwa neno “demokrasia” limetoholewa na kuendelea kutumiwa kutokea Uyunani bila kujua (au kujali) kuwa Wayunani walijifunza mfumo huu toka kwa Waafrika, ni vizuri katika muktadha wa makala hii kulichunguza neno hili kutokea Uyunani ya kale ambako mfumo wao wa kidemokrasia ulitunzwa na kuwekewa kumbukumbu vizuri zaidi kuliko ilivyokuwa kwa Afrika. Kama ilivyo kwa mambo mengine kadhaa, kumbukumbu za uasili wa Afrika hazitajwi sana. Kutokana na sababu za kutawaliwa, hasa kifikra, baadhi ya Waafrika walidharau na hawakujitahidi sana kuweka kumbukumbu na kujifunza tamaduni, mila na mienendo ya mabibi na mababu wa kale. Kwa sababu hiyo, na kutokana na mkabala wa

lugha tunaoutumia, etimolojia ya neno demokrasia itajikita zaidi kutokea huko Uyunani.

Demokrasia ya Uyunani ya kale

Demokrasia ni muunganiko wa maneno mawili ya Kiyunani (au Kigriki): *δημος* (*dêmos*) yaani watu, na *κράτος* (*Kratos*) yaani nguvu. Hapo tunapata *δημοκρατία* – (*dēmokratía*) (Diamond, 2004). Kwa tafsiri sisisi, inamaanisha nguvu iko kwa watu, au watu ni wenye nguvu. Hata hivyo, haitoshi tu kusema: “watu wenye nguvu”, au watu na nguvu. Kwa Wayunani, watu, yaani *dêmos* ilimaanisha watu wenye elimu. Ni lazima uwe na elimu ili uweze kuipata nguvu iliyolengwa na Wayunani. Kwa hiyo, unapojielimisha unajiweka katika nafasi nzuri ya kuipata hiyo nguvu. Ieleweke pia kuwa katika dhana ya demokrasia “nguvu” iliyosemwa yaani *κράτος* (*Kratos*), ilimaanisha ‘nguvu ya kuchagua’ (Nwogu, 2015: 132 - 133). Mtu mwenye elimu ana nguvu ya kuchagua. Kwa maneno mengine, Wayunani walipoliangalia neno hili, walimaanisha pia ‘nguvu ya kujua’. Yaani nguvu ipatikanayo katika elimu. Au tuseme, maana hii ya *Kratos* ilijumuisha uwezo uletwao na elimu. Ndio maana msingi mmojawapo muhimu wa demokrasia ni elimu. Yaani watu kuwa na ufahamu kuhusu jambo fulani.

Ikiwa tunakubaliana kuhusu etimolojia hii ya dhana ya demokrasia, tuingie katika misingi yake ili tuweze kufahamu vema maana halisi ya demokrasia. Msingi wa kwanza uliomo katika *Kratos*, ni ule wa uhuru wa kujua jambo ambalo halikupata kuwapo kabla (Lindell, na Scott, 1996). Mtu anapojua jambo huongeza maarifa au ujuzi.

Maarifa haya hupitia katika elimu inayompa mtu uhuru huo. Inampa mtu uhuru wa kusema jambo jipya, na kwamba, kama jambo hilo lisingesemwa, lisingejulikana. Kwa hiyo, mtu asemaye jambo hilo, sio tu huwa na uhuru wa kusema, bali pia huipata hiyo nguvu ya kusema. Ndio maana ikiangaliwa kutokea katika mantiki hii, itaonekana kuwa demokrasia sio tu mfumo wa kisiasa, wa kuchagua au kuongea, bali ni utaratibu wa kumfanya mwanajamii awe mtu kamili kwa kujua anachokiongea kwanza, na, baadaye, anachochagua. Kwa hiyo, kila mtu anastahili kujua, kuongea na kushiriki katika mfumo wa maisha ambao unamtambua yeye kama mtu kamili katika jamii. Ndio maana ni muhimu kuifahamu maana ya dhana hii inayojulikana kama “demokrasia”. Ndio maana ni muhimu kuwa na elimu kuhusu demokrasia. Elimu inakupa kibali cha kujitambua kama mtu kamili katika jamii yako. Jambo muhimu zaidi, ni namna gani unajitambua, na, ukishajitambua kama mtu kamili, ufanye nini ili kushiriki katika michakato inayohusisha demokrasia katika jamii yako.

Tumeanza kwa kuihusisha demokrasia na jamii ndogo kwanza ili tunapoanza kuiangalia ndani ya jamii pana (kama serikali) tutajua demokrasia kwa maana pana zaidi. Kutokea katika jamii ambamo msomaji anaishi, anaweza sasa kuiangalia demokrasia kama mfumo wa serikali ambamo wananchi wote wazawa wana haki sawa katika kuamua mambo ambayo yanahusu maisha na mustakabali wao. Kuamua huko huwekwa katika utaratibu kwa kutegemea jambo linaloamuliwa na wakati wa kuliama. Uamuzi huo pia unaegemea katika nguvu waliyonayo wananchi wanaoamua. Nguvu hiyo, au *Kratos* kama ilivyosemwa awali, ni ya kujua na kuweza kuamua. Nguvu ya kuchagua mfumo bora wa utawala ni sehemu mojawapo ya maana ya demokrasia, lakini sio katika ukamilifu wake.

Nguvu ya kujua namna ya kuendesha maisha ya mhusika kwa faida yake kama mwenye nchi, na kwa faida ya jamii kwa ujumla ni sehemu nyingine ya maana ya demokrasia. Maana hizi mbili hutegemeana na kukamilishana ili kuiinua jamii kwa ujumla.

Katika kuchagua namna ya kuendesha maisha, demokrasia huwa na uhusiano na sheria na kanuni. Wananchi wenye *Kratos* hujiwekea kanuni mbalimbali ambazo, tukitumia sitiari ya mimea, ni kama majani ya miti ambayo hujiimarisha katika matawi - yaani sheria, na matawi hushikiliwa au kupata nguvu zake katika shina yaani katiba. Kwa hiyo, taratibu, kanuni, sheria mbalimbali na katiba huwapo kutokana na nguvu ya ujuzi wa kielimu anayokuwa nayo mwananchi. Juu ya haya yote inaumbika demokrasia.

Kwa hiyo, tunaweza kuiangalia demokrasia kama mfumo unaoongozwa na utambuzi na ujuzi. Mfumo wa kuendesha shughuli zinazohusu maisha ya mtu, kwa makubaliano maalumu, iwe ni shughuli za ndani ya familia, kitongoji au kijiji, katika kata au tarafa, katika wilaya au mkoa. Kwa maneno mengine, na hapa ni katika muktadha wa Tanzania, ni mfumo kutoka serikali za mitaa hadi serikali kuu. Wakati fulani serikali iliamua kuwa madaraka ya “mfumo huu” yatakuwa mikoani. Hii ndiyo ilikuwa dhana ya “madaraka mikoani”.

Mtu akishindwa kufuata taratibu za nyumbani kwake, huenda pia asiweze kuheshimu taratibu za kijiji chake. Kuheshimu na kufuata taratibu ni tabia ambayo hujengwa kutokea chini katika kaya. Muundo na taratibu kadhaa katika ngazi mbalimbali huongozwa na kanuni na sheria ambazo huwa zimeandaliwa na watu wachache kwa kuongozwa na matakwa ya walio wengi. Katika mfumo huo, watu wachache huchaguliwa kuwasemea wengi

wakiyawakilisha mawazo ya hao wengi katika utaratibu maalumu. Ndio maana, kwa dhana nyepesi, demokrasia mahali pengine imetafsiriwa kuwa ni “utawala wa watu”. Ni utawala wa watu wenye nguvu za kufanya au kusababisha maamuzi yanayohusu maisha na maendeleo yao ya kila siku. Ni kwa namna gani elimu tuliyonayo inatusaidia kuipata hii *Kratos* au nguvu? Jambo hili ni la mjadala.

Msingi wa pili, mbali na ule wa “uhuru wa kujua”, ni usovereniti (Lindell, na Scott, 1996; Bassiouni na wenzake, 1998), au katika makala hii tutauita ‘ukumunsi’. Ukumunsi ni neno linalolenga kufupisha maneno ya uhuru wa kujitawala na kuwa na mamlaka na uwezo katika nchi. Nchi ikiishapata uhuru, na watu wake wakajitambua na kulitambua hilo, wakajenga utamaduni wa kujitawala na sio kutawaliwa, wakachagua watu na kuwapa mamlaka na kisha wakaheshimu mamlaka hayo, wanajipatia uwezo wa kuendeleza nchi yao kupitia mfumo ambao wote wamechangia kuufanya uwepo.

Nchi hiyo inakuwa imepata msingi muhimu wa demokrasia. Taifa lenye msingi wa ukumunsi, huitumia lugha katika ujenzi na ustawi wa demokrasia. Bila lugha, taifa haliwezi kuwa na demokrasia. Watu wake hawana lugha wala uhuru wa kuongea katika lugha yao. Vilevile, hawataweza kuchangia katika mambo yanayohusu maisha na maendeleo yao maana hakuna kuelewana kunakotokana na kutojua kile mnachotaka kuelewana. Hawawezi kuchagua watu wachache watakaowakilisha walio wengi. Taifa haliwezi kujitawala bila lugha.

Taifa haliwezi kupiga hatua yoyote ya maendeleo bila lugha. Na elimu inayowanyima watu wake misingi hii miwili, yaani, kwanza, msingi wa

uhuru wa kujua na, pili, msingi wa uwezo wa ukumuni, ni elimu ambayo haifai. Ni elimu ya kitumwa.

Katika Tanzania, jambo lingine kubwa ambalo dunia inatungalia na kutushangilia ni namna tunavyoweza sote kuwasiliana kwa kutumia lugha moja, lugha ya Kiswahili. Ni kupitia katika lugha hii, elimu ambayo ndiyo *Kratos* iwafanyayo wananchi kuwa na nguvu ya ufahamu imejengwa kupitia katika muhimili wa lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla, huwezi kuachanisha ujenzi wa demokrasia na makuzi ya Kiswahili katika Tanzania. Angalau bado katika shule za msingi watoto wanajengewa msingi huu wa kwanza katika demokrasia, msingi wa uhuru wa kujua, msingi unaowafanya waelewe kinachofundishwa, msingi unaowaenda wanafunzi kupitia lugha ya Kiswahili.

Kiswahili na ujenzi wa demokrasia

Jitihada za kuwaunganisha Watanzania wawe na lugha moja hazikujitengeneza (Blommaert, 1999). Kuna watu, wake kwa waume, ambao walifanya juhudi za makusudi kuhakikisha Watanzania wanaweza kuwasiliana bila kupitia kwa mkalimani. Watu hao ndio mashujaa wa demokrasia ya Tanzania kwa kigezo cha lugha (Besha, 1972). Walitumia njia mbalimbali kutoa elimu kwa umma kuuwezesha kusoma, kuandika na kuongea Kiswahili. Kulikuwa na uhusiano kati ya elimu, lugha na kuwapo kwa jamii yenye azma ya kujiletea maendeleo.

Kwa kutumia vyombo mbalimbali vya habari, walisambaza elimu hiyo na kuhakikisha wananchi wote wanafahamu na kukubali umuhimu wa kuwa na lugha moja (Kaniki, 1974). Walikuwa wanawapa wananchi haki yao ya uhuru wa kujua, yaani msingi wa kwanza wa demokrasia.

Habari kuhusu namna viongozi wetu walivyokitumia Kiswahili kuwahamasisha wananchi zimesemwa na wanazuoni kadhaa (Lyndon, 1969; Mwangomango, 1970; Blommaert, 1996, 1999). Kampeni mbalimbali zilizolenga maendeleo na mabadiliko katika afya ya wananchi, usafi, kuondoa ufukara, ujenzi wa nyumba bora, kuhimiza kilimo na kazi za kujenga taifa, na kuandaa dira ya Tanzania kupitia Azimio la Arusha, hayo yote yalifanyika kwa kutumia lugha ya Kiswahili (Nyerere, 1967, 1974). Vyombo mbalimbali vya habari viliwezesha mafanikio hayo. Wananchi wakawa na uhuru wa kujua kupitia elimu iliyokuwa ikitolewa, na kupata habari iliyodhamiriwa, sio tu kuwapatia uhuru wa kujua, bali zaidi kuwapatia haki ya kujitambua. Kwa hiyo, katika demokrasia kamili, lugha huambatana na habari (kupitia vyombo vya habari) kama nguzo muhimu zinazofuatana. Kupitia lugha sahihi na habari sahihi, mtu hupata urazini. Hujitambua yeye ni nani na wajibu wake ni nini katika jamii anamoishi.

Lugha ya Kiswahili imetumika kujenga na kuimarisha urazini na imekuwa ni moja ya nguzo muhimu zinazojenga demokrasia nchini Tanzania. Kupitia katika elimu, Kiswahili kimesaidia watu kupata nguvu za kiutambuzi za kuchagua wale ambao umma unawaona kuwa wanafaa kuwaletea maendeleo. Mbali na watu kufundishwa kwa Kiswahili katika shule za msingi, vitabu vya Kiswahili vimeendelea kuchapishwa vikilenga kutoa elimu katika ngazi na maeneo mbalimbali. Iwe ni elimu inayochipukia katika kazi za kubuni kama fasihi, au ni elimu kuhusu lugha na miundo yake, Watanzania wamekitumia Kiswahili kuimarisha urazini wao, kujiendeleza na kufanya maamuzi. Katika ujuzi huu, hakuna njia ya mkato. Watu wanaingia shuleni wakiwa watoto wadogo, wanafundishwa na

wanajisomea vitabu ili kupata *Kratos*. Watu wanaelezwa katika majukwaa na wanasikiliza hadithi majumbani wakijipatia *Kratos*.

Kratos—nguvu ya ufahamu na kupambanua jema na baya inapatikana kupitia elimu mbalimbali na habari zinazotolewa na vyombo mbalimbali vya habari vyenye mrengo wa kizalendo. Hata hivyo, si vyombo vyote vya habari vinaweza kusaidia kuleta demokrasia. Vyombo vya habari vya kizalendo vinatarajiwa kuwaletea wananchi demokrasia ili waweze kushiriki katika kujenga nchi yao.

Kupitia lugha ya Kiswahili, na vyombo vya habari wananchi wanapata habari, ujuzi, uwezo na nguvu ya kupanga mustakabali wao na kuchagua kuyaumba maisha kwa namna waonayo inafaa ili kujiletea maendeleo. Katika haya yote, lugha ya Kiswahili imekuwa kiungo muhimu kati ya wananchi na ujenzi wa mfumo wa kidemokrasia.

Wakati fulani, uwezo wa kufikiri wa mtu, uwezo wa kujua na kuamua, uwezo wa *Kratos*, uliingiliwa na tamaa ya pesa. Kutokana na pesa, mtu hakuwa tena na nguvu ya kujua. Urazini uletwao na *Kratos* uliharibiwa na pesa. Kwa hiyo, pesa—iwe kwa njia ya rushwa, au hongo ya aina nyingine, huingilia mchakato wa kuwapatia watu nguvu ya uchaguzi. Pesa iliwanyang'anya watu urazini wao, na pesa ilivunja utamaduni ambao ulijengwa miongoni mwa Watanzania kwa miaka mingi.

Katika shule za msingi, ilikuwa ni utamaduni watoto kujengewa uhuru wa kujua nchi na jamii zao kupitia lugha ya Kiswahili. Siku hizi, shule za binafsi zinatumia lugha ya Kiingereza (Rubagumya, 2010) kufundishia na kuwafanya watoto wadogo wawe Watanzania. Ni kwa kiasi gani lugha hii

imefumbata utamaduni na mila ya Kitanzania, ni suala la mjadala. Ni kwa kiasi gani shule hizi, kupitia katika lugha za kigeni, zinawang'oa watoto kutoka jamii inayowazunguka, nalo ni suala la mjadala mwingine. Wenye shule hizi, kile wanachokiangalia hasa ni pesa, kwa kuwa katika tafiti (Komba na John, 2015) imeonesha kuwa uelewa wa wanafunzi umeshuka. Utafiti wao unaonesha kuwa kiwango cha maarifa ni cha chini kuliko ilivyotarajiwa. Pesa imewafunga baadhi ya watu macho, imewanyang'anya urazini na kupoteza mwelekeo wa kizalendo.

Kwa hiyo, kwa serikali makini, kuivunjilia mbali tabia ya kutoa fedha, na kupokea fedha ili kushawishi maamuzi, ni njia mojawapo ya kurudisha nguvu ya kweli ya *Kratos* kwa wananchi. Wananchi walio wengi hawawezi kuwa na nafasi na nguvu ya kushiriki katika demokrasia ambayo inaongozwa na msukumo wa pesa.

Katika Azimio la Arusha, iliposemwa: “Rushwa ni adui wa haki ...” (Nyerere, 1967) maana nzima ilijikita kukataa hongo miongoni mwa wananchi. Ililenga kuwarejeshea wananchi uwezo wa kuipata haki pasipo kutanguliza pesa. Kukumbatia pesa ni kuufanya mfumo wa kidemokrasia nchini uparaganyike. Tatizo jingine la pesa ni kuvunjika kwa mhimili wa lugha ya Kiswahili uliyojenga nchi hii na kuipa jina duniani. Kabla ya Sheria ya Mabadiliko ya Elimu ya mwaka 1995, lugha rasmi ya kufundishia katika shule za msingi ilikuwa Kiswahili, ukiondoa shule chache maalumu zilizotengwa kwa ajili ya watoto wa Wanadiplomasia (Rubagumya, 2010; Komba na John, 2015). Baada ya mabadiliko hayo yaliyofuatiwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya 1995, kulitokea wimbi kubwa la uanzishwaji wa shule za awali na za msingi zilizoanza kutumia Kiingereza kama lugha ya kufundishia. Mabadiliko hayo yaliiporomoshwa, sio tu demokrasia, bali hata

kuwapo kwa Tanzania kama nchi inayoelekea kujitegemea. Badala ya kuhimiza demokrasia kwa kupendekeza lugha ya Kiswahili kutumika hata katika elimu ya juu ili kuimarisha nguzo za taifa hili, baadhi ya watu walikuwa mbioni kurudi nyuma na kuipoteza heshima na nafasi ya Tanzania katika ramani ya mataifa yanayojisimamia duniani.

Maamuzi kama haya yanaporomoshwa misingi ya demokrasia na yanaathiri maendeleo. Kama ilivyosemwa awali, misingi ya demokrasia ni pamoja na “uhuru wa kujua”. Kupitia katika lugha ya Kiingereza msingi huu si imara kwani wanafunzi hawana uhakika wanajua na hawajui nini. Kupitia katika lugha wasiyoelewa vizuri, wanafunzi wanapokonywa uwezo wa kuwa huru kujua na; kwa hiyo, wanapokonywa msingi mmojawapo wa demokrasia. Aidha, ili mtu awe na uwezo wa kuleta maendeleo, ni lazima awe na maarifa na urazini. Maarifa ndiyo chachu ya maendeleo (Georgalakis, 2017). Hivyo, kuondoa njia inayoeleweka ya kutolea maarifa ni kurudisha nyuma maendeleo ya nchi na Taifa kwa ujumla.

Kwa hiyo, upo uhusiano baina ya kuwapo kwa demokrasia na kuwapo kwa lugha inayofahamika kwa wananchi walio wengi. Haya yote yana uhusiano na maendeleo ya jamii yenye kufuata demokrasia hiyo na kwa kutumia lugha iliyo na mizizi katika jamii. Tuangalie sasa uhusiano huo wa lugha tukizingatia maendeleo ya Watanzania.

Lugha na maendeleo

Maendeleo ni mradi (Rathbone, 2014). Lugha ndiyo nyenzo kuu katika kuukamilisha mradi huu. Mazrui na Mazrui (1998) na Rathbone, (2014) wanatumia dhana ya *Mnara wa Babeli* kujadili changamoto za kuwa na lugha moja, hasa lugha katika bara la Afrika. Wanajadili ugumu uliopo

kutokana na uhusiano wa uwezekano wa lugha moja na historia ya ukoloni wa Kijerumani, Kifaransa, Kiingereza na Kireno. Katika makala hii, tunarejelea mfano kutoka katika Biblia (Mwanzo 11:1 - 9) unaoonesha kuwa wanadamu walikuwa na mradi. Kwa kuwa walikuwa na lugha moja, walielewana na kuanzisha mradi wa kujenga mji, alama yao ilikuwa ni mnara mrefu. Jamii ikiwa na lugha moja, ni rahisi kuelewana na kukamilisha “mradi” fulani. Dhana ya mradi hapa ndiyo msingi wa mjadala katika sehemu hii. Maendeleo yoyote ni mradi, na yanaweza kukamilishwa kutokana na kuelewana kwa wana mradi (Zulch, 2014), au kukwamishwa kutokana na kukosekana kwa maelewano. Katika makala hii, tunaijadili lugha ya Kiswahili na jinsi kilivyowezesha kujenga maendeleo ya kitaifa katika Tanzania.

Kama tulivyoonesha awali, mafanikio ya lugha ya Kiswahili katika kujenga maelewano katika Afrika Mashariki yalianza kwa kuikubali lugha moja, hasa baada ya mwaka 1930. Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ilifanikiwa kujenga umoja huo na kuanza kazi kubwa ya kusanifu lugha ikiegemea katika lahaja ya Kiunguja (Mbaabu, 2007). Kutokea pale, maendeleo yaliendelea taratibu kuelekea katika ujenzi wa Taifa la Tanganyika kupitia katika lugha ya Kiswahili (Blommaert, 1999). Kiswahili kikaingia rasmi maofisini na shuleni. Jamii mbalimbali zikaanza kufundishwa Kiswahili. Wanasiasa wakaanza kutumia Kiswahili katika mikutano yao (Petzell, 2012). Kutoka kuwa jamii zilizotawanyika kwa lugha na tawala mbalimbali za Kikabila, Kiswahili kikakubalika kuwa lugha moja iliyoyaunganisha makabila mbalimbali. Kiswahili kikaonekana na kuonesha kuliunda Taifa kwa jinsi kilivyopokewa na jamii tofauti zenye lugha tofauti. Kwa hiyo, muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa mwaka

1964, pamoja na mambo mengine, uliimarisha na kufanikisha ujenzi wa Taifa la Tanzania kupitia lugha ya Kiswahili (Mutembei, 2016). Kiswahili kikawa lugha iliyoandikwa katika magazeti, ikawa katika vitabu vya kusoma, na ikatumika katika nyaraka za kiofisi. Kiswahili kikawa lugha ya mdomo kuwezesha mawasiliano ya ana kwa ana, ikawa lugha ya masimulizi, na jeshini ikawa lugha ya amri za maofisa, na lugha ya kutolea hotuba za kisiasa. Kila kona, wananchi wakawa wanaunganishwa na lugha ya Kiswahili wakazidi kujiona wamoja katika taifa moja. Matendo yaliyolenga kuimarisha utaifa yalifanywa kwa lugha ya Kiswahili: michezo ya kitaifa, nyimbo za kitaifa, gwaride na kazi za kipolisi, yote yalilenga kujenga taifa moja la Tanzania. Ni vigumu kutambua maendeleo ya taifa bila ya kutaja dhima ya lugha ya Kiswahili katika kufanikisha maendeleo hayo. Maendeleo hayo hayakuwa kwa taifa tu, bali hata kwa mtu mmojammoja binafsi.

Kiswahili kilisaidia pia maendeleo ya mtu binafsi. Wananchi waliokwenda kusoma shuleni walipata elimu katika masomo kadha, na pia walipata elimu ya lugha ya Kiswahili. Walioajiriwa walikuwa pia na uwezo wa kuongea na kuwasiliana kwa Kiswahili. Ofisi nyingi za Serikali zilitaka mtumishi awe pia na uwezo wa kuongea na kuwasiliana kwa Kiswahili. Kwa baadhi ya watumishi, hasa wamisionari walitakiwa kuwa wamefanya na kufaulu mtihani wa ujuzi wa Kiswahili kabla hawajakubaliwa kufanya kazi Tanganyika, na baadaye Tanzania (Siwale na Sefu, 1977). Kwa hiyo, kufahamu lugha ya Kiswahili kukasaidia ajira ya mtu binafsi. Baadaye, wale waliokuwa na ujuzi na vipaji vya kuandika, waliendelea kama waandishi wa lugha ya Kiswahili. Walioandika mashairi, wakajulikana magazetini na kupitia radio kwa kuwa waliandika Kiswahili. Walioandika

kazi za fasihi, kama Shaaban Robert, Saadan Kandoro, Mathias Mnyampala, Kaluta Amri Abeid, kwa kutaja wachache, nao wakajulikana kwa kuwa waliandika kwa Kiswahili na kazi zao zikasomwa mashuleni. Ilipotangazwa lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa mwaka 1962, ubora na hadhi yake vikapanda katika jamii nzima.

Kampeni nyingi zilizolenga kuzindua fikra za wananchi zilifanywa kwa kutumia lugha ya Kiswahili (Blommaert, 1999). Wananchi walielewa kinachozungumzwa, wakaamua wao wenyewe na kuchagua kushiriki. Kiswahili kikatumika kuupiga vita ukabila uliotishia kuigawa Tanzania. Kwa kuwa Kiswahili kilikuwa lugha ya kufundishia katika elimu ya msingi, wananchi wengi waliyaelewa maarifa na kufurahia lugha ya Kiswahili iliyowajengea kujiona na kujisikia watu wamoja, Watanzania.

Wakati wa Azimio la Arusha, sera na harakati zote zilifanikiwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili iliandaa, na kutekeleza umiliki wa nguzo kuu za uchumi na kukuza biashara. Uendeshaji wa viwanda, mabenki, shule na elimu kwa ujumla ni miradi iliyofanikiwa kwa kuwa ilitumia Kiswahili. Mafanikio haya yalikuwapo kwa kuwa kulikuwa na mawasiliano yaliyowezesha kupitia lugha iliyofahamika kwa wote. Harakati za kilimo bora, ufugaji wa kisasa hata ujenzi wa vijiji wakati wa kampeni ya ujamaa vijijini, haya nayo yalifanikiwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Blommaert (1999:68) anakiri kuwa “ukiachilia mbali kutokuwa wazi kwa mafanikio yaliyoizunguka dhana ya utamaduni wa Ujamaa, dhima ya lugha [ya Kiswahili] ilikuwa wazi kabisa”. Hii inamaanisha kuwa matumizi ya Kiswahili yalifanikisha azma mbalimbali za serikali ukiachilia changamoto zilizojitokeza.

Wananchi walielewa kuhusu kampeni za ujenzi wa jamii mpya, na wakachagua kushiriki katika harakati za ujenzi wa jamii mpya. Kampeni nyingi zilifanywa na kufanikiwa kutokana na matumizi ya Kiswahili. Kwa mfano, kampeni dhidi ya magonjwa, vita dhidi ya njaa, harakati za kupigania uhuru wa baadhi ya nchi za kusini mwa Afrika na kushiriki katika vita ya ukombozi wa nchi hizo, hata baadaye kisomo cha watu wazima, yote haya yalifanywa na kuwezekana kutokana na mafanikio ya kukua na kuenea kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kushiriki kwa wananchi ilikuwa ni alama mojawapo iliyoonesha uhusiano baina ya lugha na maendeleo kwa upande mmoja, na lugha na demokrasia kwa upande mwingine.

Waandishi na wanasanaa mbalimbali waliunga mkono juhudi za kujenga nchi moja, taifa moja kwa kutumia lugha ya Kiswahili (Mohammed, 1971; Lodhi, 1974; Shihabuddin na Mnyampala, 1977; Bertoncini, 1994). Machapisho katika tanzu kuu za fasihi yalihimiza na kujenga umoja, kupenda ujamaa, na kuhamasisha kuhamia vijijini kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Suala la kuisitiza hapa ni ile hali ya “kuelewa” iliyoletwa na lugha ya Kiswahili. Kutokana na wananchi kuelewa kinachosemwa iwe katika kampeni au katika hotuba za kawaida za siasa, wananchi waliwezesha kushiriki katika hatua mbalimbali za maendeleo. Ushiriki wao ulitokana na ridhaa yao au uchaguzi wao, hali iliyoonesha wazi uhusiano baina ya demokrasia na lugha. Lugha inayoeleweka haikuishia katika kufanikisha hatua za kidemokrasia tu, bali pia iliwezesha kujenga mihimili ya utu. Kwa ujumla, mwananchi wa Tanzania alijenga hali ya kuwaona binadamu wengine wote ni sawa na yeye, wenye kustahili heshima ileile bila

kubaguliwa. Ahadi ya TANU ya “binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni moja” (Nyerere, 1966) ilihimiza ujenzi wa fikra ya usawa na umoja. Usawa uliojengwa ulikuwa katika ngazi tatu: Mosi, wananchi chini ya Siasa ya Ujamaa walihimizwa kuwa sawa kwa kupunguza tofauti za kipato baina yao. Jambo la pili lililoonesha usawa ni azma ya serikali kupeleka huduma za kijamii kwa watu wote mahali pote. Wananchi wote wakastahili na wakapelekewa huduma. Jambo la tatu, kupitia lugha ya Kiswahili wananchi walishirikishwa katika kufanya uamuzi. Hapa ndipo unapoonekana uhusiano wa wazi kati ya lugha na demokrasia. Lugha iliyojulikana kwa watu walio wengi ilikuwa Kiswahili. Kwa hiyo, karatasi na maelezo ya kura, yaliandaliwa kwa lugha ya Kiswahili. Wasimamizi walihakikisha wanafahamu lugha ya Kiswahili. Mambo haya matatu, yaliongelewa na Mwalimu Nyerere wakati akitathmini mafanikio na changamoto za Azimio la Arusha baada ya kupita miaka kumi, mwaka 1977 (Nyerere, 1977:12). Kwa kufanya hivi, Mwalimu aliangalia uhusiano wa demokrasia, maendeleo na haki ya mtu ya kufahamu analopaswa kufahamu na kufanya uamuzi wa kiurazini.

Hitimisho

Makala hii imeangalia uhusiano wa dhana tatu: demokrasia, lugha ya Kiswahili, na maendeleo ya wananchi. Hoja kuu ni kuwa lugha ndiyo inayoweza demokrasia, kwa upande mmoja, na kuwezesha maendeleo ya wananchi kwa upande mwingine. Hapa, kama iliyooneshwa katika makala hii, si suala la lugha tu, bali lugha inayoeleweka kwa watu wengi. Kueleweka kwa lugha kuliwafanya wananchi washiriki katika nafasi mbalimbali zilizolenga kuwapatia maendeleo. Kutumika kwa lugha inayoeleweka kulifanikisha kampeni mbalimbali za Serikali zilizolenga kuleta maendeleo katika jamii. Wananchi walielewa, na kuchukua hatua ya

kujiletea mabadiliko na wakashiriki katika kazi mbalimbali. Chaguzi nyingi walizofanya wananchi kuhusiana na kushiriki au kutokushiriki katika kazi au kampeni mbalimbali zilitokana na kuelewa kwao ni nini kilichokuwa kinahitajika. Kushiriki kwa wananchi katika uchaguzi wa viongozi ni hatua iliyoonesha kuelewa ni nini wanakifanya na kwa manufaa ya nani. Kutokea katika etimolojia ya neno “demokrasia” kwa Wayunani, tumeonesha kuwa dhana nzima iliundwa na fikra za elimu, nguvu, ufahamu na kushiriki kwa wananchi katika maamuzi. Hoja hii imeangaliwa pia katika lugha ya Kiswahili, ambapo mjadala umeonesha kuwa lugha hii imewafanya wananchi kuelewa kinachosemwa, hivyo, kufanya uamuzi wenye urazini katika kushiriki kwao kufanya maamuzi mbalimbali.

Marejeleo

Ashcroft, B. Griffiths, G. na Tiffin, H. (1995). *The Post-Colonial Studies Reader*. London, Routledge.

Ballestrin, L. (2014). Coloniality and Democracy. *Revista Estudos Políticos*: online journal Rio de Janeiro, 5(1), 210 - 228. Imesomwa Mkondoni: <http://revistaestudospoliticos.com/>.

Ramaphosa, C; Sudarsono, J; Fouraine, A; na Villoro, L. (1998). *Democracy: Its Principles and Achievement*. Publication prepared and edited by the Inter-Parliamentary Union. Parliamentary Union Geneva.

Besha, R. (1972). Lugha ya Kiswahili hivi leo; hasa katika Siasa. *Kiswahili*, 42(1), 22 - 38.

Blommaert, J. (1996). Language and Nationalism: Comparing Flanders and Tanzania. *Nations and Nationalism*, 2(2), 235 - 256.

Blommaert, J. (1999). *State Ideology and Language in Tanzania*. Koln: Rüdiger Köppe Verlag.

- Brock-Utne, B. (2002). Language, Democracy and Education in Africa: Discussion, Paper. No. 1. Uppsala, *Nordiska Afrikainstitutet*.
- Brock-Utne, na Holmarsdottir, H.B. (2004). Language Policies and Practices in Tanzania and South Africa: Problems and Challenges. *International Journal of Educational Development*, 24, 67 - 83.
- Busia, K.A. (1967). *Africa in Search of Democracy*, London: Routledge and Kegan Paul.
- Chandra, U. 2013). The Case for a Postcolonial Approach to the Study of Politics. *New Political Science*. Imesomwa kutoka DOI: 10.1080/07393148.2013.813700.
- Chatora, A. (2015). This is Africa. Mkondoni katika <https://thisisafrika.me/politics-and-society/10-quotes-from-julius-mwalimu-nyerere/>. Imesomwa Januari 2021.
- Comaroff, J.L na Comaroff, J. (1997). Postcolonial Politics and Discourses of Democracy in Southern Africa: An Anthropological Reflection on African Political Modernities. *Journal of Anthropological Research*, 53(2): 123 - 146.
- Diamond, L. (2004). What is Democracy? Imesomwa kutoka, [http://www.standard.edu/~diamond/Iraq/what is Democracy 012004.htm](http://www.standard.edu/~diamond/Iraq/what_is_Democracy_012004.htm).
- Diop, C. A. (1974). *The African Origin of Civilisation: Myth or Reality?* New York-Westport: Laurence Hill & Co.
- Elam, J.D. (2019). *Postcolonial Theory*. Imesomwa kutoka DOI: 0.1093/OBO/9780190221911-0069.
- Fanon, F. (1986). *Black Skin White Masks*. London: Pluto Press.
- Fosu, K. A. (2020). Democracy and Development in Africa. *Department of Economics Working Paper Series*. Paper: No. 26. University of Pretoria. 1 - 28.

- Georgalakis, J.; Jessani, N.; Oronje, R. and Ramalingam, B.; (wahr) (2017). *The Social Realities of Knowledge for Development*. Brighton: IDS/Impact Initiative.
- Homi, B. K. (1983). Difference, Discrimination and the Discourse of Colonialism, in *The Politics of Theory, Proceedings of the Essex Conference on the Sociology of Literature*, July 1982, Colchester: University of Essex.
- Homi, B. K. (1994). *The Location of Culture*. London: Routledge.
- Kaba, L. (1986). Power and Democracy in African Tradition: The Case of Songhay, 1464-1591. In *Democracy and Pluralism in Africa*, (ed). D. Ronen, Boulder: Lynne Rienner Publishers. 95 - 102.
- Kabongo, I. (1986). Democracy in Africa: Hopes and Prospects. In *Democracy and Pluralism in Africa*, (ed). D. Ronen, 35. Boulder: Lynne Rienner Publishers.
- Kaniki, M.H.Y. (1974). TANU: The party of Independence and National Consolidation. Gabriel Ruhumbika (ed). Towards Ujamaa: Twenty years of TANU leadership. Kampala. EALB: 1- 30.
- Kezilahabi, E. (2012). Erasure and the Centrality of Literatures in African Languages. *Kiswahili*, 75(1), 104 -117.
- Komba, S. C. na John, D. (2015). Investigation of Pupils' English Language Abilities in Tanzania: The Case of English Medium Primary Schools. *World Journal of English Language* 5(1) Imesomwa kutoka: <http://wjel.sciedupress.com> DOI:10.5430/wjel.v5n1p56.
- Konrad-Adenauer-Stiftung (2011). *Concepts and Principles of Democratic Governance and Accountability: A Guide for Peer educators*. Imesomwa kutoka: https://www.kas.de/c/document_library/get_file?uuid=56a283ae-50ff-0c9b-7179-954d05e0aa19&groupId=252038
- Lindell, and Scott (1996). *Greek-English Lexicon, Ninth Edition with a Revised Supplement 9th Edition*. Clarendon OUP.

- Lyndon, H. (1969). Language Policy in Tanzania. *Journal of the International African Institute*, 39 (3), 275 - 280.
- Magang, D. N. (1986). Democracy in African Tradition: The case of Botswana. In *Democracy and Pluralism in Africa*, (ed). D. Ronen, 103-108. Boulder: Lynne Rienner Publishers.
- Mangu, A.M.B. (2006). Democracy, African Intellectuals and African Renaissance. *International Journal of African Renaissance Studies*, 1(1), 147 - 163.
- Mazrui, A.A. na Mazrui, A.M. (1998). *The Power of Babel: Language and Governance in the African Experience*. Chicago: University of Chicago Press.
- Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Dar es Salaam, TUKI.
- Mulokozi, M.M. (2019). Pambazuko la Taaluma ya Fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki 1968 - 1980. Katika Flavia Aiello na Roberto Gaudio (wah) *Lugha na Fasihi*. Napoli. Unior Press. 19 - 31.
- Mutembei, A.K. (2016). Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar: Mjadala kupitia Lugha ya Kiswahili Sanifu. *JULACE*, 1(2), 90 - 113.
- Nwogu, G.A.I, (2015). Democracy: Its Meaning and Dissenting Opinions of the Political Class in Nigeria: A Philosophical Approach. *Journal of Education and Practice*, 6 (4), 131 - 142.
- Nyerere, J. K. (1966). *Ujamaa the Basis of African Socialism*. Dar es Salaam: OUP.
- Nyerere, J. K. (1967). *Elimu ya Kujitegemea*. Dar es Salaam: Kimepigwa Chapa na Mpiga chapa Mkuu wa Serikali.
- Nyerere, J. K. (1968). *Ujamaa Essays on Socialism*. London: Oxford University Press.

- Nyerere, J. K. (1974). *Binadamu na Maendeleo*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Onwuegbuzie, J.A., Leech, L.N, na Collins, K.M. T. (2012). Qualitative Analysis Techniques. *The Qualitative Report*. 17(56): 1 - 28. Imesomwa kutoka: <http://www.nova.edu/ssss/QR/QR17/onwuegbuzie.pdf>.
- Osabu-Kle, D. T. (2008). Western Democracy: Is it Applicable in Africa? *The Bulletin of Fridays of the Commission*, 1(3), 2 - 15.
- Petzell, M. (2012). The Linguistic Situation in Tanzania. *Moderna Språk*, (1), 136 - 144.
- Rathbone, M. (2014). Interpretations of the Tower of Babel Narrative in the African Context. *Acta Theologica*, 34(1), 173 - 196.
- Rubagumya, C.M. (2010). English-Medium Primary Schools in Tanzania: A New “Linguistic Market” In Education. Sura ya 4 katika B. Brock-Utne na wenzake. (wahr), *Language of Instruction in Tanzania and South Africa* Imesomwa Kutoka: https://doi.org/10.1163/9789460912221_005. 43 - 59.
- Said, E. (1978). *Orientalism*. London: Routledge.
- Samir, A. (1977). *Imperialism and Unequal Development*. New York: Monthly Review Press.
- Siwale, E.W. na Sefu, M.M. (1977). *The Development of Primary Education, in Tanzania*. Brock University St. Catharines, Ontario Canada. Imesomwa kutoka: <https://eric.ed.gov/?id=ED142280>.
- Stasavage, D. (2005). Democracy and Education Spending in Africa. *American Journal of Political Science*, 49 (2), 343 - 358.
- wa Thiong’o, N. (1981). The Language of African Literature, in *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. London: James Currey.

A. Mutembei

World Bank. (2006). *Managing the Implementation of Development Projects: A Resource Kit on CD-ROM for Instructors and Practitioners*. Washington DC.

Yakubu, Y. (2016). Democracy and Development in Africa the Missing Link. *International Academic Conference Proceedings*, Istanbul, 104 -111.

Zulch, B.G. (2014). Communication: The Foundation of Project Management. *Procedia Technology*, (16), 1 - 10.